



FOMU YA KUJIUNGA NA TAASISI YA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI KILIMATINDE KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

Ndugu

.....
Ninakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na Taasisi ya Afya na Sayansi Shirikishi Kilimatinde. Ninakutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya **USITAWI WA JAMII (SOCIAL WORK)** kwa Ngazi ya stashahada kwa miaka mitatu kwa mwaka wa masomo 2025/2026.

Taasisi hii ina jumla ya kozi tatu kama ifuatavyo:-

1. Kozi ya Uuguzi na Ukunga (Nursing and Midwifery)
2. Kozi ya Maafisa Tabibu (Clinical Medicine)
3. Kozi ya Maafisa Usitawi wa Jamii (Social Work)

Utatakiwa kufika chuoni siku ya tarehe 03/10/2025 kwa ajili ya kuripoti, kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni kwa siku za kazi.

1. 0. Utangulizi

Taasisi ipo katika Mkoa wa Singida , Wilaya ya Manyoni, Tarafa ya Solya na Kata ya Solya. Taasisi ipo umbali wa kilomita 18 Mashariki mwa mji wa Manyoni. Taasisi ipo ndani ya Hospitali ya Kilimatinde ambapo wanafunzi wetu hufanya mazoezi ya vitendo. Hospitali ina wataalamu wa fani mbalimbali, vifaa vya kutosha kwa mazoezi ya vitendo. Taasisi ina uzoefu wa zaidi ya miaka sitini (60) katika fani za afya. Taasisi imesajiliwa na NACTVET kwa usajili nambari **REG/HAS/024** na imepata ithibati (full accreditation) ya NACTVET. Fani zote zimesajiliwa na mabaraza ya taaluma husika. Taasisi ina wataalamu wa kutosha wenye uzoefu wa kufundisha taaluma katika fani zote.



2.0 MSINGI WA TAASISI YA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI KILIMATINDE

Taasisi ya Afya na Sayansi Shirikishi Kilimatinde inamilikiwa na Kanisa la Anglikana Tanzania (KAT) Dayosisi ya Rift Valley.

2.1 Msingi wa kwanza ni wa Kikristo, Taasisi inafuata misingi ya Kanisa Anglikana Tanzania.

2.2 Msingi wa pili ni wa elimu ya kujitegemea (**Self-reliance**) hivyo. Taasisi ina miradi ya kilimo cha mbogamboga na miti. Wanafunzi **wote** wanawajibika katika utunzaji wa miradi hiyo kwa mujibu wa sheria za Taasisi. Kila mwanafunzi atawajibika kutunza mazingira yake anayoishi.

3.0. ADA

KWA WANAFUNZI WANAOLANZA MWAKA WA KWANZA USITAWI WA JAMII (SOCIAL WORK), ADA YA MASOMO 2025/2026

Jedwali 1: Muundo wa ada

AWAMU	MUDA WA MALIPO	KIASI	
		NMB ACCOUNT 50702300049	NMB ACCOUNT 50710011059
AWAMU YA KWANZA	30/09 - 03/11 /2026	664,000/=	436,000/=
AWAMU YA PILI	15/02 - 28/02/2027	221,000/=	153,000/=
AWAMU YA TATU	15/04 - 22/04/2027	664,000/=	436,000/=
AWAMU YA NNE	01/06 - 08/06/2027	221,000/=	153,000/=
TOTAL		1,770,000/=	1,218,000/=
Grand total		2,988,000/=	

NB: Gharama hizi inajumuisha chakula, malazi, sare, Mitihani ya wizara na bima ya afya. Kumbuka, kwa kila awamu ya malipo, pesa inayotakiwa kulipwa itawekwa kwenye akaunti mbili tofuti kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo juu.

JINSI YA KULIPA

NB: Unatakiwa kuandika majina yako kamili ya usajili kwenye risiti yako ya malipo (pay slip). Pia utoe nakala kwa ajili ya kumbukumbu yako.

ADA YA MASOMO ILIPWE KWENYE AKAUNTI ZA TAASISI ZIFUATAZO:

NMB ACCOUNT 50702300049; Jina la account ni: **KILIMATINDE NURSES TRAINING SCHOOL** au Utapewa control namba kwa ajili ya malipo.

NMB ACCOUNT 50710011059 Jina la account ni: **KNTS DEVELOPMENT ACCOUNT.**

NB: Mwanafunzi anapaswa awe amemaliza kulipa fedha zote za ada ya muhula mmoja kabla ya kuanza muhula mwingine, vinginevyo hataruhusiwa kufanya mitihani ya mwisho wa muhula huo.



4.0 SHERIA ZA TAASISI KWA UJUMLA

4.1 Taasisi inafuata sheria za Wizara ya Afya, pia Taasisi imejiwekea sheria ndogo ndogo katika mazingira yake ambazo mwanafunzi anapaswa kuzifuata.

4.2 Wanafunzi wa kike wanaruhusiwa kusuka nywele kulingana na mwongozo wa mavazi wa wizara ya afya, lakini hawaruhusiwa kusuka nywele za bandia, wanafunzi wa kiume hawaruhusiwi kufuga nywele na ndevu, wanafunzi wanapaswa kunyoa nywele ziwe fupi

4.3 Mwanafunzi anaweza kushindwa kuendelea na masomo/kufukuzwa shule kwa sababu zifuatazo:

- a. Akishindwa mitihani na ikiwa maendeleo yake hayaridhishi kwa kufuata mwongozo wa mtaala husika
- b. Kushindwa kutii sheria za taasisi ambazo atapewa na kutia saina pindi anapofika chuoni.
- c. Kushindwa kufuata taratibu na miongozo ya mitihani mbalimbali
- d. Kuonyesha tabia isiyoendana na maadili ya kazi za afya.
- e. Sababu za kiafya ambazo zitamfanya asimudu masomo yake.

5.0. MITAALA

Taasisi inatumia mitaala ya mafunzo kutoka Wizara ya Afya na iliyoidhishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

6.0. VITU AMBAVYO MWANACHUO ANATAKIWA KUJA NAVYO WAKATI WA KURIPOTI:

- a. Cheti cha kuzaliwa – original
- b. Vyeti halisi vya secondary (Original certificates)
- c. Masweta mawili MEUPE yasiyo na maandishi wala picha (masweta yenye kofia hayaruhusiwi kabisa)
- d. Shuka 4 na foronya 2 (shuka 2 pinki na blue bahari 2).
- e. Ndoo ndogo mbili yenye ujazo wa lita 10.
- f. Rubber squeezer 1
- g. RIM Paper mbili (2) size A4 Mondi No. 1 uzito 80g/m²
- h. Picha ya passport size 2
- i. Nguo za binafsi, Mavazi yote yawe ya heshima kumbuka Taasisi yetu ya Mafunzo ya Sayansi za Afya ni Taasisi ya Kanisa na ipo kijijini ambapo mavazi kama **suruali** kwa wasichana, nguo fupi na zilizobana hazikubaliki katika jamii hii. Suruali za **jeans** kwa wavulana hazaruhusiwi kabisa hapa chuoni na muda wote wa mafunzo.
- j. Viatu vyeusi vya ngozi jozi (pair) mbili vyenye visigino vifupi visivyotoa sauti wakati wa kutembea sakafuni na viatu vya michezo wakati wa michezo.



- k. Soksi zinazoruhusiwa kwa wasichana ni soksi ndefu nyeupe jozi tatu na kuendelea na Soksi zinazoruhusiwa kwa wavulana ni soksi nyeupe jozi tatu na kuendelea.

7.0. SARE ZA TAASISI

Sare zilizokubaliwa na Wizara katika vyuo vya Afya ni:-

- Mwanachuo atatakiwa kuvaa sare zitakazoshonwa chuoni kufuatana na mwongozo wa Wizara ya Afya na Wizara ya Usitawi wa Jamii. Hii ni kulingana na taaluma husika unayosomea na jinsi ilivyoainishwa na baraza la taaluma.
- Mwanafunzi atatakiwa kuja na Viatu vyeusi vya ngozi jozi (pair) mbili vyenye visigino vifupi visivyotoa sauti.
- Soksi jozi tatu na kuendelea. **Wasichana rangi Nyeupe ndefu, Wavulana rangi Nyeupe.**

8.0 UCHELEWAJI.

Tunakushauri uwahi siku ya kuanza chuo, ukichelewa zaidi ya siku 14 hutaruhusiwa kusajiliwa. Mwanafunzi atapata likizo ya wiki 4 kila mwaka na akichelewa baada ya likizo atawajibishwa kulingana na taratibu zilizopo za wizara na Taasisi.

NB: Kama kuna sababu maalumu, mzazi/mlezi atoe taarifa chuoni, na kama ni ugonjwa, mwanafunzi aje na cheti cha Daktari cha hospitali alikotibiwa na inayotambulika.

9.0 MSIBA.

Ikiwa kwa bahati mbaya mwanafunzi atapata msiba, mzazi anatakiwa kutoa taarifa kwa uongozi wa Taasisi na si mwanafunzi (mtoto wake). Uongozi wa Taasisi utamfahamisha mwanafunzi huyo aliyepata msiba. Mwanafunzi anaruhusiwa kushiriki kwenye msiba wa watu wafuatao:-

- Wazazi (Baba/Mama) au walezi
- Kaka na Dada wa kuzaliwa
- Mtoto wake
- Mume/Mke
- Ndugu wa karibu

Principal's Signature and Stamp

The Principal
Anglican Diocese of Rift Valley
Kilimatinde Institute of Health
and Allied Sciences
P.O. Box 43, Manyoni



KWA UPOLE NA HOFU (1 Petro 3: 15)



FORM No. III: MEDICAL REPORT FORM

PART I: PERSONAL PARTICULARS (To be filled by the candidate)

SURNAME: OTHER NAMES

AGE SEX

COURSE OF STUDY

MARITAL STATUS

(PART II –V to be filled by a medically qualified and registered professional)

PART II: (PERSONAL HISTORY): Are you suffering or have you suffered from any of the following? Indicate YES or NO.

1. Tuberculosis
2. Asthma
3. Rheumatic fever
4. Allergic disorder
5. Heart disease
6. Gastric or duodenal ulcers
7. Jaundice
8. Dysentery
9. Varicose veins
10. Kidney disease
11. Diabetes
12. Epilepsy
13. Deformity
14. Mental illness
15. Eye disorder
16. Ear, nose or throat disorder
17. Skin disease
18. Anaemia



19. Gynaecological disorder.....
20. Any other serious disorder(specify).....

PART III: PHYSICAL EXAMINATION

1. Height (cm).....
2. Skin
3. Weight (kg).....
4. Eyes: Conjunctivae Pupils.....
- Vision With glasses: Right..... Left:.....
- Vision Without Glasses: Right..... Left:.....
5. Ears (state if any discharge)
6. Mouth and throat
7. Nose:
8. Cardiovascular system Blood pressure: Systolic..... Diastolic
- Heart: any mummer? Arteries and veins
9. Respiratory system
- Lungs fields
10. Abdomen

PART IV: LABORATORY/RADIOLOGY

1. Urine: Albumin.....
- Sugar
- Leucocytes.....
- Schistosoma.....
2. Stool, Special emphasis should be on hookworms or schistosoma.
3. Blood examination
- a. HB level e. Lymphocytes.....
- b. Neutrophils..... f. Monocytes.....
- c. Eusinoiphils..... g. ESR.....
- d. Basophils.....
4. Serology.....



Pregnancy test (female)

Widal test (VDRL)

5. X – ray examination – Chest (**include radiological report**).....

PART V: CONCLUSION

I have examined Mr/Miss/Mrs..... and consider that he/she is physically and mentally fit to be admitted to the Institute for diploma studies.

Date:

Signature

Name:

Title:

Qualifications:

Official STAMP